# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

# TAARIFA KWA UMMA

## TAARIFA YA MAKUSANYO YA KODI KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI – MACHI, MWAKA WA FEDHA 2024/25

**Dar es Salaam, 03 Aprili, 2025**

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ninapenda kuutaarifu umma kuwa katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2024/25 (Januari – Machi , 2025), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi Trilioni 7.53** sawa na ufanisi wa **asilimia 101.32** ya lengo la kukusanya **Shilingi Trilion 7.43,** ambao ni sawa na ukuaji wa **asilimia 13.47** ukilinganisha na kiasi cha **Shilingi Trilioni 6.63** zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2023/24, kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1.**

**Jedwali Na. 1: Makusanyo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa Mwezi Januari - Machi, 2024/25**

***Shilingi Trilioni***

| Mwezi | Makusanyo 2023/24 | 2024/25 | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Lengo | Makusanyo | Ufanisi | Ukuaji |
| Januari | 2.12 | 2.38 | 2.42 | 101.68% | 13.81% |
| Februari | 2.02 | 2.26 | 2.27 | 100.23% | 12.25% |
| Machi | 2.49 | 2.79 | 2.84 | 101.90% | 14.16% |
| **Jumla** | **6.63** | **7.43** | **7.53** | **101.32%** | **13.47%** |

***Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania***

Makusanyo yaliyokusanywa katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2024/25 yanapelekea Mamlaka ya Mapato Tanzania kuweza kuweka **rekodi ya kipekee katika utekelezaji wa majukumu yake kwa KUFIKIA NA KUVUKA LENGO LA MAKUSANYO KWA MIEZI TISA MFULULIZO KATIKA MWAKA WA FEDHA.** Katika kipindi cha mwezi Julai – Machi, mwaka wa fedha 2024/25, Mamlaka ya Mapato Tanzania imekusanya kiasi cha **Shilingi Trilioni 24.05** sawa na ufanisi wa **asilimia 103.62** ya lengo la kukusanya **Shilingi Trilioni 23.21,** na ukuaji wa **asilimia 17.01** ukilinganisha na kiasi cha **Shilingi Trilioni 20.55**. Aidha, makusanyo haya ni ya kiwango cha juu kabisa kufikiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kipindi kama hicho toka

kuanzishwa kwake, na ni sawa na ongezeko la **asilimia 77** toka kiasi cha **Shilingi Trioni 13.59** zilizokusanywa katika kipindi kama hichi mwaka wa fedha 2020/21, **Miaka minne toka Mhe. Dkt. Samia suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aingie madarakani.**

Ufanisi huu katika makusanyo uliofikiwa mwezi Julai – Machi mwaka wa fedha 2024/25 ni matokeo chanya ya kutekeleza kwa vitendo maagizo na maelekezo ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** yanayohusiana na uongezaji wa uhiari wa ulipaji kodi kupitia uboreshaji wa huduma kwa walipakodi na uboreshwaji wa shughuli za biashara nchini.

Hatua zilizochukuliwa na kufanikisha ufanisi wa makusanyo katika kipindi cha Julai – Machi, mwaka wa fedha 2024/25 ni pamoja na:

**1.** Kutekeleza Miongozo na Maelekezo ya Mh. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kuhamasisha ulipaji Kodi wa Hiari nchini.

**2.** Kuongezeka kwa utendaji kazi mzuri, nidhamu na ubunifu kazini kwa watumishi wote wa Mamlaka ya Mapato, kwa kutekeleza yafuatayo:

**A.** Kuendelea kuimarisha mahusiano na ushirikiano na Jumuiya za wafanyabiashara pamoja na wafanyabiashara wote nchini na Kuendelea kutoa elimu ya kodi kwa njia mbalimbali kwa wafanyabiashara wote nchini;

**B.** Kuanza matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Forodha (TANCIS) ulioboreshwa, uliozinduliwa mwezi Januari 2025, ili kuimarisha usimamizi wa vyanzo vyote vya mapato vya Forodha;

**C.** Kufuatilia kwa ukaribu hali ya ufanyaji biashara nchini kwa kusimamia kikamilifu uzalishaji wa viwandani pamoja na kuendelea kuhimiza matumizi ya mashine za kielektroniki (EFD) nchini;

**D.** Kuendelea kuweka kipaumbele katika utoaji wa huduma bora zinazozingatia mahitaji ya walipakodi, kuwahudumia walipakodi siku za mapumziko (Jumamosi na Jumapili) kupitia ofisi zote za TRA nchini;

**E.** Kuendelea kuboresha mahusiano na wafanyabiashara na kutatua changamoto za biashara kwa kutenga siku ya Alhamisi ya kila wiki kuwa ni siku maalum ya ***'Kusikiliza Walipakodi'*** kupitia ofisi zote za TRA nchini.

**F.** Kuongezeka kwa ulipaji kodi wa Hiari nchini kutoka miongoni mwa walipakodi.

**3.** Kuendelea kutekeleza mikakati na kampeni za uhamasishaji wa uhiari wa ulipaji kodi nchini.

**4.** Serikali kuendelea kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji nchini, hali iliyopelekea:

**A.** Kuongezeka kwa shehena ya mizigo inayoingizwa au kuondoshwa nchini katika vituo vya Forodha nchini, kufuatia uimarishwaji wa huduma zitolewazo bandarini;

**B.** Kuendelea kuongeza mahusiano baina ya Mamlaka ya Mapato Tanzania na wawekezaji kupi tia njia za majadiliano na mikutano; na

**C.** Kuendelea kuongezeka kwa idadi ya **Waendesha Uchumi Walioidhinishwa** *(Authorized Economic Operators)* nchini

Katika kufanikisha ukusanyaji wa mapato katika miezi iliyobaki ya mwaka wa fedha 2024/25 (Aprili - Juni), Menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania inaendelea kutekeleza kikamilifu mambo yafuatayo:

**1.** Kutekeleza maagizo yote ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu usimamizi wa kodi nchini na uhamasishaji wa ulipaji kodi kwa hiari;

**2.** Kukamilisha ujenzi wa moduli zote za Mfumo wa Usimamizi wa Kodi za Ndani (IDRAS) ifikapo Juni 2025;

**3.** Kuendelea kuimarisha mahusiano na ushirikiano na walipakodi kupitia utoaji wa huduma bora pamoja na kampeni za elimu kwa mlipakodi;

**4.** Kuendelea kuimarisha usimamizi wa utoaji wa risiti za kielektroniki za EFD nchini kupitia kampeni mbalimbali za uhamasishaji, pamoja na kuwakumbusha wananchi juu ya umuhimu wa utoaji wa risiti za kielektroniki za EFD kwenye maendeleo ya nchi;

**5.** Kuendelea kusimamia na kuimarisha misingi ya mfumo mzuri wa kodi, ikiwemo Haki na Usawa katika utozaji kodi (no favouritism or victimization) ili kuweka mazingira ya biashara yaliyo sawa;

**6.** Kushirikiana kwa kikamilifu na timu iliyoteuliwa na **Mheshimiwa Rais** inayofanya mapitio ya mfumo wa utozaji kodi nchini ili kuleta maboresho makubwa katika mifumo ya kodi nchini;

**7.** Kuimarisha na kusimamia weledi (professionalism) na huduma nzuri kwa walipakodi (customer service) ikiwemo watumishi wetu wote kuvaa vitambulisho muda wote wanapotoa huduma; na

**8.** Kuimarisha vitengo vya Ukaguzi na Uchunguzi wa Kodi ili Kuzuia ukwepaji kodi za ndani na Forodha na kuondoa upotevu wa mapato ya Serikali ili kuweka mazinigira ya biashara yaliyo sawa kwa wafanyabiashara wote.

Menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania INAPENDA KUWASHUKURU WALIPAKODI WOTE walioweza kutimiza wajibu wao kwa kulipa kodi stahiki kwa wakati na kuendelea kuunga mkono kizalendo juhudi za Serikali za kuleta maendeleo nchini kwani “Kodi Yetu Ndiyo Maendeleo Yetu”.

**Mwisho,** kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), napenda kuwatakia nyote Sikukuu njema za Eid na Pasaka.

***“Pamoja Tunajenga Taifa Letu”***

Yusuph Juma Mwenda
**Kamishna Mkuu**